

Kuhamasisha Kupitia kwa Vyombo vyat Habari

Washiriki watajifunza kuhusu na kutambua njia ambazo aina mbalimbali za vyombo vyat habari huweza kutumiwa kutoa uhamasisho kuhusu suala fulani.

Kutumia Vyombo vya Habari kwa ajili ya kuleta Mabadiliko

Sehemu ya Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Vyombo vya habari ni zana bomba ya kushiriki mawazo pamoja na watu wengine. Watu wengi hupendelea majukwaa ya vyombo vya habari ya kidijitali kuwasiliana ujumbe wao. Kwa mfano, HolaSoyGerman hutumia YouTube kushiriki na watu kote duniani hadithi za kuchekesha naye Malala Yousafzai hutumia Twitter kutetea haki za kina mama na watu wenye umri mdogo.

Wakati mwengine, watetezi wenye umri mdogo hutumia vyombo vya kidijitali kulenga matatizo mahususi. Kwa mfano, Amandla Stenberg ni mwigizaji mwenye umri mdogo na ni mkereketwa ambaye alitoa video mnamo 2015 kuhusu utamaduni wa watu weusi na kuanza kutumika kwa tamaduni za jamii zilizotengwa katika darasa lake la historia. Kwa kutoa video hiyo, alikuwa kama mtetezi na akasambaza habari kuhusu tatizo ambalo anafuatilia kwa dhati. Watu wengine wanapendelea kutumia vyombo vya habari vya jadi, visivyo vya kidijitali kama vile Televisheni, redio au magazeti kuwaambia hadhira fulani kuhusu mawazo yao.

Kwenye kiwambo kikubwa kilicho sehemu ya mbele ya chumba, onyesha mfano wa video ya hivi majuzi inayoambatana na muktadha wako / au muktadha wa mtaani wa mshiriki / au wa kikanda ili kueleza zaidi jinsi vyombo vya habari vinaweza kutumiwa kusambaza habari na katika utetezi kuhusu shughuli fulani.

Ambia Wanafunzi Wako

Kama watetezi wa mabadiliko, vyombo vya habari vya aina zote vinaweza kuwa zana muhimu sana katika kufikia malengo yetu. Katika shughuli hii, mtachunguza wazo hili kwa kuandaa ujumbe na kusambaza kwenye aina mbalimbali za vyombo vya habari ili ufikie hadhira pana.

Kazi

Sehemu ya Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Tafuta mfano wa maudhui (k.v video kwenye YouTube, chapisho la Facebook, picha) yanayohamasisha na huenda yakawa njia nzuri ya kusaidia kusambaza ujumbe kuhusu shughuli unayofuatilia kwa dhati. Utatumia muda wa dakika 15 kutafuta maudhui haya. Baadaye, kila mshiriki ataonyesha kikundi kile walichopata na kwa nini wanafikiria kwamba kinahamasisha.

Mwingiliano wa Darasa

Wape washiriki dakika 15 ili watafute mfano wa maudhui ambayo wanaamini kwamba yanasmabaza ipasavyo ujumbe kuhusu shughuli fulani. Baadaye, chukua dakika 15 na umuulize kila mshiriki afafanue na / au aonyeshe video yake kwenye kikundi kwa kifupi na kujadili sababu zao za kufikiria kuwa maudhui hayo yanahamasisha.

Sehemu ya pili ya kazi hii inaweza kukamilika wakati wa kukutana wakati wa sasa au kikundi cha pili, kulingana na muda uliotengwa.

Sehemu ya Pili

Ambia Wanafunzi Wako

Kwa vile sasa tumepeata na tukajadili mfano unaohamasisha na unaofaa wa maudhui ili kuendeleza shughuli fulani, sasa ni wakati wenu kuandaa maudhui yenu binafsi yanayohusu shughuli mnayofuatilia kwa dhati. Katika muda wa dakika 20 zijazo, tafakari kuhusu shughuli ambayo ni muhimu kwako na unakili wazo lako kuhusu aina mahususi ya maudhui ya kutumiwa kusambaza habari kuhusu shughuli hiyo. Mawazo haya yanaweza kujumuisha:

1. Chapisho la matini la kuwasiliana kuhusu shughuli yako na kwa nini watu wanafaa kuchukua hatua.
2. Wazo kuhusu picha au mchoro (au picha / mchoro wenywewe) ili kuwasiliana kuhusu shughuli yako na jinsi watu wengine wanavyoweza kuisaidia.
3. Wazo kuhusu video ili kuhamasisha na kuhimiza hatua ichukuliwe kuhusiana na shughuli hiyo.

Pamoja na wazo hili, tafadhali pia andika:

1. Angalau njia mbili unazoweza kutumiwa kusambaza ujumbe wako wa midia ili kuongeza uonekanaji na uhamasisho wa sababu yako.

Mwingiliano wa Darasa

Wape washiriki dakika 20 ili waandike hoja zao. Baadaye, waulize washiriki kushiriki kile wameandika kwenye kikundi kikubwa. Chukua dakika 15 kufanya mjadala.